# Mabadiliko makubwa yanayolenga wakimibizi, waomba hifahdhi, walio na kibali cha TPS na wahamaiji wengine

## ADA MPYA NA DAI YA JUU KWA WAKIMBIZI

Mnamo Julai 4,2025, Rais Trump alitia Saini **muswada mmoja mkuu maridadi (One Big Beautiful Bill Act (OBBBA)** )kuwa sheria.Hii sheria kuu ya ufadhili inatoa msukumo mkubwa kwa utekelezaji wa uhamiaji na zaidi **pia kuongezea ada nyingi zinazohusiana na uhamiaji**, inayaweza kuleta ugumu kwa wengi kufikia au kuendelea na mchakato wao wa uhamiaji.

Hapa ni kati ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara (FAQs) kuhusu jinsi mabadiliko haya yataadhiri wateja wa IRC:

### Nina omba kuwa mkaaji wa kudumu(LPR) na USCIS, haya mabadiliko ya ada yana maanisha nini kwangu?

Ada **za kubadilisha hali yako kuwa LPR na USCIS** kwa kawaida huanzia **$1,440** kwa watu wazima, lakini **baadhi ya watu hawahitajiki kutoa ada yoyote**, wakiwemo wakimbizi, SIVs, wahamiaji maalumu vijana, na wengineo. OBBBA haiongezi ada mpya kwa walengwa hawa amabao tiyari wamepewa wameondolewa dai la ada wanapotuma ombi.

Kama **unatuma ombi kupitia mahakama ya uhamiaji(au EOIR)**, OBBBA inaweka **nyongeza ya ada** ya $1,500 juu ya ada ya $1,050 ya EOIR , jumla **ni $2,940**, kwa baadhi ya watuma ombi. Tafadhali zungumza na mwakilishi wako wa kisheria kuelewa ada kamili kuhusiana na ombi lako la LPR.

### Ninataka kuomba uhifadhi. Je, ninatajika kulipa ada?

Ikiwa unatuma ombi kwa **USCIS** au **EOIR**, kwa sasa lazima ulipe ada **ya $100 kwa ombi la kwanza kuuliza uhifadhi na $100 ya kusubiria jibu kwa mwaka** , ya kila mwaka ombi lako la uhifadhi linapokuwa katika hali ya kusubiriwa. Ada hii inatarajiwa kila tarehe uliotuma ombi lako k.m ikiwa ulituma ombi Julai 29,**2025**, itabidi utume $100 isiyoweza kurudishwa pamoja na 1-589, tarehe ya Julai 29, **2026**, USCIS au EOIR lazima wapokee $100 ada yako ya kila mwaka ya "kusubiria" uhifadhi.

### Mimi ni mwomba hifadhi na ombi langu linasubiria mahakamani. Je hii ina maanisha nini kwangu?

Kwa sasa kuna **malipo ya $100 kila mwaka** ya kusubiria ambayo ungehitaji kulipa **kesi yako ya uhifadhi inaposubiria** . EOIR haijatoa mwelekezo jinsi ya kulipa ada hii kama tiyari umetuma ombi la ufadhiri kwa mahakama ya uhamiaji. Kwa wale wanotuma ombi(bila kupitia mahakama ya uhamiaji)USCIS inakupa mwelekeo na kutia notisi binafsi kwa watu na taarifa kuhusu linina vipi ada zitalipwa, na matokeo ya kukosa kulipa ada zinazotarajiwa za mwaka. Maelekezo kuhusu ada pitwa za mwaka huu kutoka USCIS zinatarajiwa karibuni. Lakini inatumainiwa waomba unhifadhi wanatarajiwa kulipa ada ya mwaka kabla ya tarehe hitimisho tangu ulipotuma ombi lako

### Je, na kuhusu ada ya kadi ya kukubaliwa kufanya kazi?

Kwa wale wanaomba uhifadhi, TPS na wasamehewa, kuna ada za juu kuomba kibali cha kutumika kazi. Tazama jedwali hili kwa maelezo ya kidani

### Je, patakuwa na mabadiliko ya ada tena?

Ada **inaweza kubalika kila mwaka wa makadilio ya fedha** na tangazo litatolewa kupitai tovuti ya EOIR au USCIS

### Mabadiliko ya ada ya kutuma ombi ya USCIS ,mahakama ya uhamiaji (EOIR) na Bodi ya Rufaa ya Uhamiaji(BIA)

| KITENGO | MABADILIKO YA ADA YA OMBI LA USCIS* | MABADILIKO YA ADA YA OMBI LA EOIR NA BIA. |
|---|---|---|
| WAOMBA UHIFADHI<br>(Fomu I-589) | **$100**(isiyoweza kurejeshwa na haina msamaha). **Ada ya mwaka ya kusubiria:$100** kila mwaka wakati ombi lako la uhifadhi linaposubiriwa. | **$100**(isiyoweza kurejeshwa na haina msamaha). **Ada ya mwaka ya kusubiria:$100** kila mwaka wakati ombi lako la uhifadhi linaposubiriwa. |
| VIBALI VYA KUTUMIKA KAZI(EAD)<br>(Fomu I-765) | **Kwa TPS na waomba msamaha**<br>• **Kibali cha kutumika kazi cha kwanza kwa TPS nawaomba msamaha $550** kwa waomba uhifadhi, au wapewa msamaha,au watuma ombi wa TPS, na ada zaidi ya USCIS jumla **$1,020** kupitia mtandao, au **$1,070** ikitumwa kama barua.<br>• **Kuongeza muda: $275 kila wakati,** kwa kibali kwa sasa zikiwa na **muda wa mwaka mmoja tu**, na ada zaidi ya USCIS ya sasa, jumla ikiwa **$745 kupitia mtandao au $795** ukitumia fomu ya ombi<br>**Kwa Waomba hifadhi**<br>• **Kibali cha kutumika kazi cha kwanza $550**<br>• **Kuongeza muda: $275 kila wakati**, kwa kibali kwa sasa zikiwa na **muda wa mwaka mmoja tu**, na ada ya USCIS ya sasa, jumla ikiwa **$745 kupitia mtandao au $795** ukitumia fomu ya ombi<br>**Kwa Wenye hifadhi**<br>• Hamna mabadiliko ya ada ( hamna ada ya kwanza au ya kuongeza muda wa EAD kwa wale waliopewa hifadhi) | |
| OMBI LA MKAAJI HALALI WA KUDUMU(LPR)<br>(Fomu I-485) | Hamna mabadiliko ya ada kama unatuma ombi kwa USCIS. | EOIR inaweka tabaka tofauti za ada mpya kuwa ada ya $1,500 juu ya ada ya awali ya $1,050 jumla ni **$2,940,** kwa baadhi ya watuma ombi. Tafadhari zungumza na mwakilishi wako wa kisheria kuelewa ada kamili kuhusiana na ombi lako la LPR. |
| ADA YA KUTUMA OMBI YA TPS<br>(Fomu I-821) | Kwa sasa $500(zaidi kutoka takriban $50), hamna masamaha wa ada, USCIS itatoza ada zaidi za kutoa alama za vidole, jumla **$530**. | Kwa sasa $500(zaidi kutoka takriban $50), hamna masamaha wa ada, USCIS itatoza ada zaidi za kutoa alama za vidole, jumla **$530**. |
| RUFAA | | Kuna nyongeza ya $900 juu ya ada ya awali ya $110,nyongeza zaidi kwa sasa kuwa jumla ya **$1010,isipokuwa rufaa ya uwekezaji ambayo haina ada**. |
| HOJA YA KUFUNGUA TENA AU KULIFIKIRIA UPYA MBELE YA EOIR<br>(KWA MSAMEHEWA WACHACHE) | | **$1,045**(ilikuwa takriban $110 au bure) |
| HOJA YA KUFUNGUA TENA AU KULIFIKIRIA UPYA MBELE YA BIA | | Kuna nyongeza ya $900 juu ya ada ya awali ya $110,nyongeza zaidi kwa sasa kuwa jumla ya **$1010** |
| ADA KAMA UMETIWA MBARONI BAADA YA KUKOSA KUFIKA KORTINI | | **$5,000** kama umetolewa hukumu ya kuvurushwa kwa sababu ya kutofika kortini na umetiwa mbaroni baadaye.Hamna msamahama kama amri ya mahakama imeondolewa. |

**Tahadhari:** Pale USCIS imeongeza ada, imeratibiwa **kuanza Agosti 21, 2025**, mabadiliko ya **EOIR yanaaza mara moja**. Mashirika yote mawili yanaweza kuongea ada zaidi.

*Kwa taarifa maalum, rejelea tovuiti ya [USCIS fee calculator.]

### Ada zingine mpya

| | |
|---|---|
| **Kama umetiwa mbaroni mipakani** | **$5,000** kama umekamatwa ukivuka Katikati ya vivuko halali mipakani. Haieleweki hatua za kuendelea kama umeshindwa kulipa ada mara moja |

ILISASISHWA MWISHO, AGOSTI 12, 2025

INTERNATIONAL RESCUE COMMITTEE

*Rasilmali hii inatoa Habari ka jumla tu na si ushauri wa kisheria. Mtarajio ya ada za uhamiaji na mwelekeo inabalika kwa kasi. kwa taarifa ya wakati huu na mwelekezo maalumu kuhusu kesi yako, zungumza na wakili wa uhamiaji au zungumza na mahakama husika ya uhamiaji moja kwa moja.*